MARAIS Moi wa Kenya, Nyerere wa Tanzania na Obote wa Uganda katika mkutano wa Kihistoria uliofanyika Arusha ambapo msingi mpya wa ushirikiano kati ya nchi hizi tatu ulizinduliwa.
PICHA: KNA

PONGEZI: RAIS MOI, NYERERE

HATUNA BUDI kutoa pongezi maridhawa kwa Watukufu Marais Wet watatu Wanaoongoza Mataifa ya Afrika Mashariki na Kati, Rais Daniel arap Moi wa Kenya; Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Tanzania na Rais Daktari Milton Obtoe wa Uganda kwa kufikia maafikiano yatakayokuwa ya manufaa kwa wananchi wa nchi hizi zetu.

MARA baada ya kupokea habari za mkutano maalum wa Arusha nchini Tanzania, ambapo ndipo palipokuwa na Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, wananchi wa nchi hizi tatu walikuwa na hamu kubwa ya kujua ufumbuzi na maafikiano juu ya mazungumzo yao na hakuna aliyetegemea kama kuna jambo zuri lolote litakaoafikiwa.

LAKINI kutokana na busara za viongozi wetu - Rais Moi, Nyerere na Obote - walifikia maamuzi ambayo yana manufaa na yatakayoleta matunda mema kwa wananchi wa nchi hizi za Mashariki ya Bara letu la Afrika. Jumla ya yote kuna mengi ambayo yameonyesha dalili njema siku za usoni.

Jambo kubwa na la maana zaidi liloafikiwa kwenye mkutano huo ni uamuzi wa Rais Moi na Rais Nyerere wa kufungua mipaka ya nchi zao; mipaka ambayo ilikuwa imefungwa kwa miaka karibu sita iliyopita na kabla ya hapo ilikuwa mwananchi wa Kenya ama Tanzania hawezi kuvuka isipokuwa apate kibali cha kumruhusu kufanya hivyo.

TUKIFIKIRIA tutokapo na tuendapo, dalili njema imechipuza na tuna uhakika viongozi wetu wenye busara na taaluma ya kutosha ya kujuwa wanayoyataka wananchi wao, watayatimiza ipasavyo na kuona wananchi wa Afrika Mashariki na Kati wanaendelea kuwa ndugu kama walivyokuwa kabla ya ubaya ambao hatuutaki tena, kuzuka!

MUNGU ibariki Afrika Mashariki, Uwabariki na Viongozi Wake! - **ABDULRAHMAN SHERIFF**

WANANCHI WA KENYA NA TANZANIA WAFURAHI MIPAKA KUWA WAZI

VIONGOZI kadha wa Serkali, kundi la Thalatha Twaifa pamoja na wananchi kadha walishangalia uamuzi uliochukuliwa na Marais wa nchi mbili za Kenya na Tanzania za kufungua mipaka iliyokuwa imefungwa kwa miaka sita iliyopita, na pia wakaeleza matumaini yao kuhusu kurudishwa kwa uhusiano baina ya mataifa yote ya Afrika Masariki na Kati.

NA ABDULRAHMAN SHERIFF

Katika taarifa na risala za pongezi kwa viongozi wa nchi tatu za Afrika Mashariki, Rais Moi wa Kenya, Mwalimu Nyerere wa Tanzania na Daktari Milton Obote wa Uganda, ambazo zinaendelea kumiminika kutoka sehemu kadha za mkoa wa Pwani katika afisi ya *COASTWEEK*, wananchi hao wameeleza furaha zao kuhusiana na mapatano ya Arusha.

Meya wa Jiji la Mombasa, Diwani Ahmed Shahame Mwidani alisema katika risala yake kuwa wakati umefika kwa wananchi wa nchi hizi tatu kujumuika na viongozi katika kurudisha uhusiano mwema na undugu uliokuwako hapo awali. "Hapana shaka Afrika Mashariki itapiga hatua kubwa ya maendeleo kutokana na mapatano yaliyofikiwa huko Arusha", akasema Diw. Mwidani.

Akiwasifu Marais Moi, Nyerere na Obote kwa busara waliyotumia ya kukuatana na kujaribu kurudisha angalau uhusiano mwema baina ya mataifa haya, Tamimu wa Thalatha Twaifa, Sheikh Mohammed Salim Shirazy alimwambia ripota wetu kuwa viongozi hao wametambua yale wananchi wa nchi zao wanayoyataka katika kujifikiria kama ndugu.

Bw. Shirazy alisema: "Wananchi wa Kenya, Tanzania na Uganda ni watu waliozaana na kuoana na ilikuwa shida sana kutembeleana wakati wa harusi ama wakati wa shida. Hatuna budi kuwashukuru viongozi wetu kwa kutuwezesha tena kutembeleana na kujuliana hali".

Tamimu huyo wa Thalatha Twaifa alisema kufunguliwa kwa mipaka baina ya Kenya na Tanzania kutasaidia sana wananchi wa nchi hizi mbili kuwasiliana na kurudisha undugu waliokuwa nao toka enzi za vizazi vilivyopita. Alifikiria kuwa biashara kati ya nchi mbili zitazidi kuimarishwa.

Bw. Shirazy alikariri matamshi ya Mtukufu Rais Moi ya Kuwaomba wananchi wa nchi mbili za Kenya na Tanzania kuwa macho juu ya maovu yoyote yatakayofanywa kuhusiana na nchi hizo. "Hatuna budi kuangamiza maovu yoyote ambayo yanaweza kutokea na kuleta uhusiano mbaya kati ya nchi zetu mbili", akamaliza Bw. Shirazy.

Naye Diw. Laban makonjero wa Likoni pamoja na Diwani Maalum, Diw. Khamis Mabee walipongeza hatua iliyochukuliwa na Rais Moi, Obote na Nyerere na wakawa na maoni uhusiano kati ya nchi hizi mbili utazidi kuimarishwa na kutiliwa mkazo.

Kutoka huko Dar es Salaam nchini Tanzania, wananchi nao pia walizipokea habari za kufunguliwa mpaka na Kenya kwa furaha kupita kiasi na baadhi ya wananchi hao waliwasiliana na *COASTWEEK* na kueleza vile sherehe zilivyokuwa wakati wa kutangazwa kwa habari hizo njema.

Bw. Mwindadi Sheha wa mtaa wa Magomeni mjini Dar alisema: "Hakika tumejiona kama tuko huru kutokana kwa uamuzi wa viongozi wetu. Sisi wananchi tuna furaha kubwa na hatuna budi kuwa wamoja na kuzidi kuwapa viongozi wetu mioyo ya kupendana.

MSASANI

Naye Babu Taib Manswab Allui na nduguye, Bi Shammim Manswab wa Msasani walisema wamekosa kuwatembelea wazazi wao wanaoishi Mombasa kwa kipindi cha zaidi ya miaka 11 na sasa: "tuna furaha kwani tutaweza tena kwenda Mombasa kuwaona wazazi wetu".

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA T-SHIRT KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD No. 175

KWENDA KULIA:

1. Ardhi iliyopandwa maua na miti ya matunda.
5. Umoja wa mataifa.
6. Si nene.
7. zanzibar.
8. Nusu ya Baba.
10. United Kingdom
12. Mbwa mkubwa
14. Sehemu isiyoota nywele.
15. Asili ya tunda.
16. Funga nikahi.
17. Zana za kufanyia kazi fulani.

KWENDA CHINI:

1. Chombo cha jikoni cha udongo.
2. Kitu cha chuma cha kufungia mlango.
3. Mwenda tezi na omo maregeo ni ....
4. Aina ya samaki wa bahari.
5. Uji mzito wa mtoto mchanga.
9. Tamko la kukataa.
10. Chombo chakutolea maji katika dau.
11. Kiumbe cha ufuoni.
12. Mahali pa taka.
13. Mti wa mtama au mahindi

Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 174

1. **Shahida** B. Sanduku La Posta **113, VOI.**

2. Mrs. Fatma Abubakar, Sanduku La Posta 85026, MOMBASA.

3. Habiba Abdalla, Sanduku La Posta 83360, MOMBASA.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 174

KWENDA KULIA

1. AKATAMBUA, 5. AMBIRI, 7. RIA, 8. LA, 9. JA, 10. ATHI, 11. SI, 13. MFU, 15. SHABABU 17. IMBA, 18. VOI.

KWENDA CHINI

1. ASALI, 2. TARATIBU, 3. BURA, 4. AMANI, 6. BA, 9. JIMBI, 11. SU, 12. CHOO, 14. FUMO, 16. ZAO.



JINA...................................

SANDUKU LA POSTA...................................

....

Shindano la Fumbo La kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipe**lekwe** kwa Muharriri *COASTWEEK*, Sanduku la Posta **87270**, Mombasa, Kenya. **Siku** ya jumatano tarehe **Dec. 14 1983. Saa** nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.

RAIS MOI ATIA SAHIHI KITABU CHA DUMILA.

*Mtukufu **Rais Moi** hivi majuzi alikipokea kitabu cha "NYAYO ERA AND CULTURE na kukitia sahihi, jambo ambalo limemtia hima kubwa mwandishi wake, Faraj Dumila. Baadaye katika tamasha ya karamu ya Waandishi wa Magazeti, huko Hotel Hilton, Waziri Mdogo, Bw. Erik Khasakhala ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Utamaduni nchini alivipokea vitabu hivyo viwili kutoka kwa mwandishi wake an kumpongeza kwa juhudi yake ya kueneza utamaduni hasa juu ya kuwatia wavulana na wasichana wakuze kipawa chao cha Uandishi wa Fasihi ya Kiuzalendo.*

Bw. Dumila hivi sasa yuko katika harakati za kutayarisha kitabu cha tatu cha "Nyayo Era and Culture" ambacho chatarajiwa kutoka siku ile ya kusherehekea mwaka wa ishirini tokea Kenya ijipatie Uhuru wake, mnamo tarehe kumi na mbili, mwezi wa Desemba, 1983.

*Nakili hii inaeleza mengi kuhusu njia kudumisha mapenzi ya nyumbani na kurudia kupiga chapa ile insha inayopendwa sana na wasomaji nayo ni "Thermometer of Love" yaani "Kipimo cha Mapenzi" na pia "Glimpses of Love" yaani "Vidokezo vya Mapenzi". Kuna Insha Kubwa Juu ya **Maongozi** ya Nyayo na Uzalendo. Waandishi wa magazeti na watangazaji wanaelezwa umuhimu wao wakati huu wa ujenzi wa nchi na kusherehekea siku huu hiyo ya mwaka wa Ishirini.*

Pichani Mwandishi Faraj Dumila (kushoto) akimkabidhi Bw. Erik Khasakhala nakala ya vitabu hivyo katika sherehe ya Hilton Hotel.